**12A-Swifaatu Dhawaatil-adhwdaad (Swiffah Zilizo Na Kinyume)**

**A- صِفَاتُ ذَوَاتِ الأَضْدادِ Swifaatu Dhawaatil-adhwdaad (Swiffah Zilizo Na Kinyume)**

1. **الْهَمْسُ Al-Hams - Kunong'ona**[1] na kinyume chake ni **الْجَهْرُ Al-Jahr – Kusikika;** Swiffah hizi zina athari ya sauti.

| الْهَمْسُ<br>**Al-Hams**<br>**(Kunong'ona)** | الْجَهْرُ<br>**Al-Jahr**<br>**(Kusikika)** |
|---|---|
| Kutoa pumzi yaani sauti ya kunong'ona inayotoa upepo wakati wa kutamkwa herufi katika herufi za al-hams. Herufi zake ni kumi (10) zimekusanywa katika ibara:<br>فَحَثَّهُ شَخْصٌ سَكَتَ<br>Ukiweka mkono mbele ya mdomo ukatamka herufi hizi, utahisi hewa kutoka mdomoni. Jaribu kutamka herufi zifuatazo:<br>أَفْ فَ فُ فِ | Kuzuia kutoka pumzi yaani kutokutoa sauti ya kunong'ona wakati wa kutamkwa herufi. Herufi ni zilizobakia ukizitoa herufi zisizokuwa za al-hams.<br>أ ب ج د ذ ر ز ض ط ظ ع غ ق ل م ن و ي |

[1] Kutokana na upana wa lugha ya Kiarabu, maana za Swiffah huenda zikawa si kama zilivyokusudiwa lakini nimejaribu kuzipa maana za karibu kabisa, na itahitaji mwalimu kufafanua zaidi.

2. الشِّــــدَّة **Ash-Shiddah** –**Nguvu** na kinyume chake ni الـرَّخـاوَة **Ar-Rakhaawah** - **Udhaifu** na baina yao iko **At-Tawassutw** الـتَّـوَسُّـــط – **Wastani.**

| الشِّدَّة **Ash-Shiddah (Nguvu)** | التَّوَسُط **At-Tawasswutw (Wastani)** | الرَّخَاوَة **Ar-Rakhaawah (Dhaifu)** |
|---|---|---|
| Kuzuia kutoka kwa sauti wakati wa kutamkwa herufi miongoni mwa herufi za ash-shiddah. Mfano ت katika خُلِقَتْ<br><br>Herufi zake ni nane (8) zimekusanywa katika ibara:<br><br>أَجِدُ قَطٍ بَكَتْ | Swiffah iliyopo baina ya ash-shiddah na ar-rakhaawah kwa maana; sauti haizuiliki kikamilifu wala haiendelei kikamilifu bali huwa kati na kati.<br><br>Herufi zake ni 5 zilizokusanywa katika ibara:<br><br>لِنْ عُمَر | Kutangulia kutoka sauti wakati wa kutamka herufi miongoni mwa herufi za ar-rakhaawah. Mfano ش katika مَعَايِش<br><br>Herufi zake ni zote zilobakia ukitoa herufi za ash-shiddah na at-tawassutw<br><br>ث ح خ ذ ز س ش ص ض ظ غ ف و ه ي |

3. الإِطْبَاق **Al-Itwbaaq – Kufunga** na kinyume chake ni الإِنْفِتَاح **Al-Infitaah** - **Kufungua;** Swiffah hizi zina athari ya sauti

| الإِطْبَاق<br>**Al-Itwbaaq**<br>**(Kufunga)** | الإِنْفِتَاح<br>**Al-Infitaah**<br>**(Kufungua)** |
|---|---|
| Kukutana sehemu ya ulimi na sakafu ya juu ya mdomo (kufungika) wakati wa kutamka herufi. Swiffah hii huilazimu herufi kufungika hata ikiwa ina *i'raab* ya kasrah. Herufi zake ni nne (4) zenye nguvu kabisa.<br>ص ض ط ظ | Kutenganisha baina ya ulimi na sakafu ya juu ya mdomo wakati wa kutamka herufi na hivyo mdomo hufunguka. Herufi zake ni herufi zote zisizokuwa za al-itwbaaq<br>أ ب ت ث ج ح خ د ذ ر ز س ش ع غ ف ق ك ل م ن و هـ ي |

4. الإسْــتِعْلاء **Al-Isti'-laa – Kupaa juu** na kinyume chake ni الإسْــتِفال **Al-Istifaal – Kuinamisha**[2] Hizi ni swiffah za lazima ambazo haziepukani na dhati ya herufi. Swiffah hizi zina athari ya sauti

| الإسْتِعْلاء<br>**Al-Isti'-laa**<br>**(Kupaa juu)** | الإسْتِفال<br>**Al-Istifaal**<br>**(Kuinamisha)** |
|---|---|
| Kuelekeza shinikizo ya herufi (hewa yake) kwa kupandisha ulimi juu ya sakafu ya mdomo wakati wa kuitamka herufi na kujaza mdomo. Herufi zake ni saba (7) zilizokusanywa katika ibara:<br>خُصَّ ضَغْطٍ قِظْ | Kuteremsha ulimi chini wakati wa kutamka herufi yaani kutokufanya mdomo kujaa. Herufi zake ni herufi zote zisizokuwa za ألإسْــتِعْلاء (al-isti'laa).<br>أ ب ت ث ج ح د ذ ر ز س ش ع ف ك ل م ن و هـ ي |

---

[2]Inajulikana pia kama ni Tafkhiym na Tarqiyq – Tafkhiym na Tarqiyq ni matokeo ya Swiffah ya ألإسْــتِعْلاء (al-isti'laa) na الإسْــتِفال (al-istifaal)l, hivyo Tafkhiym na Tarqiyq ni Swiffah "Aaridhwah" za kuzuka.

5. **الإِذْلاق Al-Idhlaaq – Mtiririko** na kinyume chake ni **الإِصْمَـــــات Al-Iswmaat – Kuzuilika**; swiffah hizi hazina athari ya sauti[3]

| الإِذْلاق<br>**Al-Idhlaaq**<br>**(Wepesi na uharaka)** | الإِصْمَات<br>**Al-Iswmaat**<br>**(Kuzuilika/Uzito na ugumu)** |
|---|---|
| Wepesi na uharaka wa kutamka herufi kwa sababu ya kutoka kwake kutoka ncha ya ulimi au midomo miwili. Imeitwa hivyo kwa kuwa baadhi yake hutoka ukingoni mwa ulimi, nazo ni: ر ن ل na baadhi yake hutoka kutoka midomo miwili, nazo ni: ف م ب Herufi zake zimekusanyika katika ibara: فَرَّ مِنْ لُب | Kuhitajika juhudi ya kuzitamka herufi na hutamkwa polepole na kutoka ndani ya mdomo na koo. Herufi zake ni herufi zote zisizokuwa za al-idhlaaq<br><br>أ ت ث ج ح خ د ذ ز س ش ص ض ط ظ ع غ ق ك و هـ ي |

**Tanbihi:** Swiffah hizo zote zinakuwa na nguvu zaidi herufi zinapokuwa zina sukuwn, na zinapunguka zinapokuwa na *i'raab*.

[3] Zinahusiana na Swarf katika lugha ya Kiarabu.